

Nafasi ya Sitiari katika Mabadiliko ya Kisemantiki ya Leksia za Kiswahili: Ulinganisho wa Kiswahili cha Kabla ya Karne ya Ishirini na Kiswahili cha Kisasa

Tirus Mutwiri Gichuru, Ireri Mbabu na Kitula King'ei
Chuo Kikuu cha Kenyatta, Kenya

Ikisiri

Makala haya yamejadili nafasi ya sitiari katika mabadiliko ya kisemantiki ya leksia za Kiswahili kwa kulinganisha mifano mahususi ya Kiswahili cha kabla ya Karne ya Ishirini na Kiswahili cha Karne ya Ishirini na Moja. Aidha, imeshughulikia mahusiano kati ya maana za leksia za awali na za kisasa. Makala pia imejadili athari za sitiari katika muundo wa lugha ya Kiswahili. Asili ya data iliyochanganuliwa ni kutoka kwa matini teule za kabla ya Karne ya Ishirini na kutoka kwa wazungumzaji wenye elimu-asilia. Uchanganuzi umeonyesha bayana kuwa mbinu ya sitiari imekuwa muhimu katika kubadilisha maana za leksia na pia muundo wa kisemantiki wa Kiswahili, katika kipindi kilichotafitiwa. Pindi jamii nzima ilivyobadilika kutokana na maendeleo ya sayansi, teknolojia, uchumi, kijamii na kisiasa, ndivyo pia lugha ya sitiari mpya zinazidi kuchipuka.

Maneno Muhimu: Sitiari, mabadiliko, semantiki, leksia

Utangulizi

Utafiti wetu wa hivi majuzi umethibitisha kauli ya Lakoff (1987) kuwa kuwa ‘sehemu kubwa ya lugha inayotumika na binadamu ni sitiari’. Sitiari ni utaratibu wa kuhamisha maana toka kitu au dhana moja hadi kitu au dhana nyingine (Kahigi 1995). Kwa Wanasemantiki Tambuzi kama vile Lakoff (*ibid*) lugha huhusisha ujenzi wa picha za mawazo na mipaka ya kidhana katika mawanda ya kiutambuzi. Basi kwao, sitiari ni mchakato wa kuhamisha dhana kutoka kwa wanda moja na kuichopeka kwa dhana tofauti ya wanda jingine. Katika mfanyiko huu, leksia fulani yenye maana yake bainifu hutumiwa kurejelea dhana nyingine kwa njia fiche. Kwa mfano *kipusa* (upembe wa thamani wa kifaru) kutumiwa kama sitiari ya *msichana mrembo*.

Maumbile na umbo lake binadamu humjengea binadamu misingi ya kutambua dhana mbalimbali katika mazingira yake kupitia picha au taswira

(Vyvyan et al 2006, Lemmens, M. 2017). Kwa mfano, mtoto anaanza kuelewa dhana ya ‘ndani na nje’ kuititia tajriba yake ya kuweka vitu ‘ndani ya’ mdomo wake. Matumizi ya hisia za binadamu yaani kuona, kusikia, kuonya, kunusa na hisia ya mguso humjengea misingi inayomsaidia kuufafanua ulimwengu halisi na wa kidhahania kisitiari; hali ambayo husababisha mabadiliko ya kisemantiki. Mabadiliko yanapotokea huwa na athari katika muundo wa lughha.

Mbinu za Utatfiti

Data iliyochanganiuliwa ilikusanywa kutoka kwa matini za kale za Kiswahili na nyingine kukusanywa kutoka kwa wahojiwa walio na ujuzi wa Kiswahili cha kale. Matini zifuatazo ziliteuliwa Krapf, J. L. (1882) *Dictionary of Suaheli Language* Steere, E. (1870): *A Handbook of the Swahili Language as Spoken at Zanzibar. Revised Edition by Madan* (1919), Burt, F. (1910) *Swahili Grammar and Vocabulary*, Hichens William (1939): *Al-inkishafi; The Soul's awakening*, Allen J.W. T (1971): *Tendi: Six examples of a Swahili Classical Verse form with Translations and Notes*, Abdulaziz Mohammed H. (1979): *Muyaka 19th Century Swahili Popular Poetry*, Mutiso wa Kineene (2005) *Utenzi wa Hamziya*, M.M. Mulokozi (mhariri) 1999: *Tenzi Tatu za Kale*, Chiraghdin S.(1987) *Malenga wa Karne Moja na Nabhany*, S. A. (2012): *Kandi ya Kiswahili*.

Kati ya leksia mia tano zilizokusanywa, sampuli ya leksia mia mbili ilianishwa na kupangwa katika makumbo ishirini na matatu kwa misingi uhusiano wa kimaana. Kwa mfano, leksia za wanyama, leksia za vifaa, leksia za biashara na kadhalika. Leksia za Kiswahili cha kale kilichofifia na zingine ambazo zingali zinatumika katika Kiswahili cha kisasa k.v. *umeme*, *kanga* na *ndege*.

Uchanganuzi na Matokeo

Ili kufanikisha uchanganuzi na kuboresha uwasilivu, uchanganuzi ulizingatia makumbo anuwai kwa kufafanua historia ya mabadiliko ya kila leksia na kuambatanisha na maelezo kuhusu mbinu za kisemantiki zilizohusika katika mabadiliko husika. Mtindo huu umependelewa kwa kuwa ulisaidia kupunguza uziada wa kujirudiarudia. Ilibainika kuwa mbinu za mabadiliko ya kisemantiki hazina uzito sawa katika kuathiri maana za leksia. Ilibainika kuwa mbinu zalishi zaidi ilikuwa upanuzi wa maana iliyohusisha asilimia 64% ya jumla ya leksia zilizochanganuliwa. Ilifuatwa na mbinu ya **sitiari (30%)**, usogezi wa maana (21%), udhalilikaji (15%), usfinyizi (07%), tasfida (06%), uimarikaji (05%), sinedoche (03%), metonimu (03%) na chuku (01%). Asilimia 58 ya leksia zilizochanganuliwa zilihuisha zaidi ya mbinu moja ya mabadiliko. Makala haya yamejikita katika mbinu ya sitiari. Ili kufikia malengo ya makala haya, mifano ya leksia imeteuliwa kutoka katika makumbo tisa ambayo imewakilisha leksia zilizobadilika kisitiari.

(a) Leksia za Sanaa na Mawasiliano

Hizi ni leksia za kutajia vifaa na dhana mbalimbali zinazohusiana na sanaa na mawasiliano katika jamii ya kale ya Waswahili. Hii hapa ni mifano ya leksia zilizobadilika kisitiari:

(1)

<i>Leksia</i>	<i>Maana asilia</i>	<i>Maana mpya ya kisitiari</i>
Upembe	Mfupa ulio kichwani (wanyama)	Umbo lolote lenye ncha k.v. ~ wa Afrika.
Msuko	Sanaa ya kupitisha chane au nywele	Ploti au mtiririko wa vitushi, bahari ya shairi
Buye	Mchezo wa kufungana macho	Dhana au hali ya neno kutodokeza maana
Ubaa	Pande la mti lililopasuliwa	Kifaa cha kuandikia kwa jiwe la grieve au chaki > kifaa kipana cha rangi nyeusi cha kuandikia kwa chokaa nyeupe >kifaa chochote cha kuandikia cha plastiki, karatasi maalum n.k.

Ni bayana mabadiliko ya kisitiari yamepanua mipaka ya utambuzi ya leksia husika.

(b) Leksia Zinazohusiana na Nyumba na Vifaa vyake

Leksia za nyumba pia zimetumiwa kisitiari kuwakilisha dhana mpya. Hii hapa ni mifano:

(2)

<i>Leksia</i>	<i>Maana asilia</i>	<i>Maana mpya ya kisitiari</i>
Nyumba	Jengo panapoishi watu	Familia au watu wa mbari moja. Ndoa
Lango	Mlango mkubwa wa jengo	Familia au nasaba. Mahali pa kufungia mpira. Kiingilio chochote halisi au cha kidhhanania.
Kiingilio	Mahali pa kuingilia jengoni	Ada inayotozwa wanaoingia mahali fulani k.v. kujiunga na klabu au chama, michezoni au sinema.
Jiko	Mahali pa kupikia	Mke, Oa
Dirisha	Mwanya ukutani	Kiolwa windo cha wastani katika tarakilishi ambacho huangazia data.

Katika karne ya ishirini, leksia *behewa* ilimaanisha *chumba mojawapo cha ndani katika jumba la Kiunguja* (Krapf 1884:24). Krapf (keshatajwa) aliambatanisha behewa na vyumba vya watu wa Unguja tu. Hata hivyo, maana ya ‘behewa’ iliyokuwa ya awali zaidi iliyokopwa kutoka Kiarabu. ilikuwa ‘eneo la wazi lisilo na dari ambalo limezungukwa na majengo ya nyumba’. Mabadiliko yalichukua mkondo ufuato:

Eneo la wazi lisilo na dari ambalo limezungukwa
na majengo ya nyumba



Chumba mojawapo cha ndani katika jumba la
Kiunguja (Kabla ya karne ya 20)



Vyumba, bohari na sehemu ya garimoshi ya
kubebea abiria na mizigo (Karne ya 20 - 21)

Katika kisasa leksia hii huwakilisha *vyumba, bohari na sehemu ya garimoshi ya kubebea abiria na mizigo*. Huenda mabadiliko haya yalitokea kati ya miaka 1896 hadi 1902 wakati wa ujenzi wa reli ya Uganda ulifanyika ukiongozwa na Mwandisi George Whitehouse kwa ufadhili wa Uingereza. Huu ni upanuzi wa maana kisitiari.

(c) Leksia za Mavazi

Leksia za mavazi pia zimetumiwa kisitiari kuwakilisha dhana mpya. Hii hapa ni mifano:

(3)

<i>Leksia</i>	<i>Maana asilia</i>	<i>Maana mpya ya kisitiari</i>
Kanga	Nyuni mwenye madoadoa	Kitambaa cha kujifunga kiunoni na mabegani; leso
Kitambi	Vazi la Kiunoni	Tumbo lililochomoza mbele kwa unene
Mtumba	Furushi la nguo	Kilichotumiwa na mwengine (secondhand items)

Iteleweke kuwa leksia *kanga* hupatikana katika lugha zingine za Kibantu k.v. *ŋkanga* Kimeru, *ŋganga* Kikuyu. Leksia hii ingali inatumika katika Kiswahili Sanifu kwa maana hii hii (Taz. TUKI 2013:191). Kulingana na National Museums of Kenya (2005) katika *Swahili Attire “Exhibition”*, kuna ithibati ya kutosha kuwa miaka ya 1800 katika eneo la Mombasa na Unguja kulizuka leso maarufu na za kuvutia zilizokuwa na michoro na rangi iliyoshabihiana na ya ndege (*kanga*). Basi Waswahili wakaziita leso husika ‘*kanga*’. Kuanzia mwaka wa 1920, kampuni ya *Kaderdina Hajee Essak Ltd*, Mombasa ilianza kuandika semi na methali katika *kanga*. Hadi miaka ya 1950 maandishi yaliandikwa kwa

hati za Kiarabu. Maandishi kwa hati za Kirumi yalianza 1960. Hatimaye watu walihamisha maana kutoka wanda moja hadi lingine kisitiari kuwakilisha dhana mpya.

(d) Leksia za Zinazohusiana na Vita

Kuna leksia za kivita ambazo zimepata maana mpya kupitia mbinu ya sitiari. Hii hapa ni mifano:

(4)

<i>Leksia</i>	<i>Maana ya awali</i>	<i>Maana mpya ya kisitiari</i>
Mzinga	Kifaa cha mviringo cha kufugia nyuki	Chombo cha cha kupigia risasi. Kitu hodari, -zuri au hatari. Juma ni ~
Kifaru	Mnyama mwenye upembe usoni	Gari la kivita lenye mzinga usoni
Kiboko	Mnyama mnene wa pori	Mtu mnene, mjeledi

Vifaru vilitumiwa kwa mara ya kwanza na Ufalme wa Muungano wakati wa vita vya kwanza vya dunia (1914-1918) dhidi ya Wajerumani. Basi mabadiliko ya leksia hii huenda yalitokea wakati huo.

(e) Sehemu za Mwili

Leksia za sehemu za mwili pia zimetumiwa kisitiari kuwakilisha dhana mpya. Maumbile na umbo lake binadamu humjengea binadamu misingi ya kutambua dhana mbalimbali katika mazingira yake, kile wanaisimu tambuzi huita pitcha au taswira (Vyvyan n.w. 2006; Lemmens, 2017). Hii hapa ni mifano:

(5)

<i>Leksia</i>	<i>Maana asilia</i>	<i>Maana mpya ya kisitiari</i>
Macho	Kiungo cha kuona	Pambo linaliwekwa katika omo au gubeti ya jahazi
Ulimi/Ndimi	Kiungo kilicho kinywani	Lugha mbalimbali, msimbo
Mdomo	Sehemu ya kuingizia chakula	Sehemu ya kuingizia vitu ~ <i>wa chupa</i>
Tumbo	Mfuko wa kusagia chakula	Katikati ya umbo ~ <i>la meli,</i> ~ <i>la gari</i>
Kichwa	Sehemu ya juu ya mwili	Katikati ya kiwiliwili Kiongozi, mada kuu ya

		taarifa, injini ya gari moshi ambayo hukokota mabehewa
Shavu	Sehemu iliyoko chini ya sikio	Pande mbili za mwanya wa kuma

(f) Leksia za Vyakula na Mazao

Leksia za vyakula na mazao pia zimetumiwa kisitiari kuwakilisha dhana mpya. Hii hapa ni mifano:

(6)

<i>Leksia</i>	<i>Maana ya awali</i>	<i>Maana mpya ya kisitiari</i>
Banzi	Kipande cha mti uliochanjwa	Aina ya chakula Kiitwacho chipsi.
Unga	Nafaka iliyosagwa	Dawa ya kulevyaa kama vile ‘heroine’
Mtindi	Maziwa gande au yaliyotolewa siagi	Pombe. Nahau piga ~ (kunywa pombe).

Katika mifano (6) inabainika wazi kuwa mabadiliko husika ya kisitiari si ya kiholela bali yanaongozwa na taswira za mwono na mwonjo.

(g) Leksia Zinazohusiana Mazingira

Leksia zinazohusiana na mazingira pia zimetumiwa kisitiari kuwakilisha dhana tofauti na kusababisha upanuzi wa leksia husika. Hii hapa ni mifano:

(7)

<i>Leksia</i>	<i>Maana asilia</i>	<i>Maana mpya ya kisitiari</i>
Ulingo	Jukwaa la kulindia shamba	Jukwaa la michezo, taaluma ~wa siasa
Umeme	Mwangaza mkali kabla ya radi	Mwangaza au nguvu za stima au betri
Uga	Uwanja wazi wa kuchezea	Elementi katika jedwali la tarakilishi (field)
Maji	Kiowevu kipatikanacho mitoni	Pombe, Wizi wa mitihani (Kenya)
Tuta	Mwinuko wa kupanda viazi vitamu	Mwinuko barabarani wa kupunguza kasi

(h) Leksia za Mimea

Leksia za mimea pia zimetumiwa kisitiari kuwakilisha dhana mpya. Hii hapa ni mifano:

(8)

<i>Leksia</i>	<i>Maana asilia</i>	<i>Maana mpya ya kisitiari</i>
Msasa	Mti wenyе majani yanayokwaruza	Karatasi ya kulainisha mbao.
Mzizi	Sehemu ya mmea iliyoko ardhini	Nyoosha mambo yaliyoharibika.
Kiini	Moyo au sehemu iliyono ndani kabisa	Kipashio cha neno ambacho hakwezi kuvunjwa zaidi bila kupoteza utambulisho
Tawi	Sehemu ya mti itoayo majani.	Undani wa jambo, kisa au tukio, chanzo.
		Sehemu ndogo ya chama au shirika

(i) Leksia za Wanyama

Tunatumia leksia wanyama kuwakilisha ndege, wanyama na wadudu.

(9)

<i>Leksia</i>	<i>Maana asilia</i>	<i>Maana mpya ya kisitiari</i>
Ndege	Nyuni	Chombo cha kusafiria angani
Kifaru	Mnyama wa porini	Gari la kivita
Kipusa	Upembe wa kifaru	Msichana mrembo, kidosh
Kupe	Mdudu anyonyaye damu	Mtu au taifa linalotegemea jingine
Kipanya	Mnyama mwenye mkia mrefu	Kiteuzi cha tarakilishi
Beberu	Mbuzi wa kiume	Mkoloni, mtu mchafu

Mabadiliko haya si ya kiholela bali yalitokana na mshabaha wa utendakazi kati ya dhana zote mbili. Mbinu ya sitiari inatawaliwa na vigezo muhimu vinavyojenga uhusiano kati ya leksia ya awali na leksia badiliko.

Mahusiano ya Kisitiari

Mabadiliko ya kisitiari si ya kiholela; huwa na vigezo mbalimbambali vinavyodhibiti mageuko husika. Kwa kweli katika mchakato wa kuhamisha dhana kutoka kwa wanda moja na kuichopeka kwa dhana tofauti ya wanda jingine, mshabaha wa aina fulani unaokitwa katika tambuzi za wanaojua lugha husika huhusishwa. Hisia za kuona, kugusa, kusikia, kuonja na kunusa ni muhimu katika kuhusisha dhana na ishara mbalimbali katika ulimwengu wake. Kwa mfano, anayeona chombo cha angani *ndege* atatambua kwa wepesi ina sifa zinahusiana na za ndege licha ya kuwa katika wanda tofauti. Uchunguzi wetu ulibainisha mahusiano yafuatayo ya kisitiari:

(i) Uhusiano wa Kiumbo na Kimaumbile

Huu ni uhusiano wa kihistoria unaotokana na kuhusisha umbo au umbile halisi au la kidhahania la dhana A na la dhana B. Kwa ufupi B ina asili katika A. Maumbile na umbo lake binadamu humjengea binadamu misingi ya kutambua dhana mbalimbali katika mazingira yake, kile wanaisimu tambuzi huita pitcha au taswira (Vyvyan et al 2006). Zingatia mifano katika jedwali lifuatalo:

Jedwali 1: Uhusiano wa Leksia Kiumbo

Leksia	A	B	Uhusiano wa A-B
Ndege	Nyuni	Chombo cha angani	Kuwepo kwa mbawa za kupaa angani
(m)lango	Kiingilio cha nyumba au mji	Mahali pa kufungia bao katika soka	Kuwepo kwa mwanya wa kuingilia
Umeme	Mwangaza mkali unaoandamana na ngurumo wakati wa mvua, radi	Nguvu za stima au betri	Kutoa mwangaza mkali
Shavu	Pande mbili za uso, chini ya jicho mpaka karibu na taya	Sehemu ya uke; pande mbili	Maumbile
Mzinga	Mzinga wa nyuki	Silaha	Umbo la mviringo.

Maana za leksia katika B zina historia yake katika A. Kwa mfano neno *ndege* (chombo cha kusafiria angani) lina uhusiano wa kihistoria na *ndege* (nyuni) ambaye alitanguliwa kuwepo katika mazingira ya Kiswahili. Basi kuwepo kwa umbo A ndio msingi wa kuwepo kwa umbo B.

(ii) Uhusiano wa Kimatumizi

Huu ni uhusiano wa kihistoria unaotokana na dhana ya matumizi. Kwa mfano, *mkono* wa tingatinga una uhusiano wa kihistoria na *mkono*; sehemu ya mwili ya kushika. Pia maana ya awali ya *ulingo* (mahali palipoinuka shambani palipotumiwa kulindia mazao yasiharibiwe na ndege au wanyama) katika (Krapf 1882) ndio asili ya leksia ya kisasa *ulingo* ambayo ni sitiari ya kutajia *mahali au wanda linalotumika kwa shughuli maalum, maarifa au taaluma*.

Aidha, maana ya awali ya ‘kinu’ ni ‘kifaa cha mti au mawe chenyе kina kilichotumiwa na Waswahili kutwangia nafaka, kubondea mizizi ya kutengeneza dawa na kusindikia mafuta. Kijiti cha kutwangia kinaitwa mche. Katika kisasa leksia hii imepata maana zingine za ziada. Hutumiwa kutajia *mtambo au mashine ya kutengeneza vidhaa k.v ~ cha usumba, ~cha soda, ~cha kusagia nafaka (mashine ya kusagia), ~cha kuzalisha umeme n.k.* Uhusiano wa leksia mpya na wa awali ni wa kimatumizi.

(iii) Uhusiano wa Kitabia/Sifa

Huu ni uhusiano wa kitu na kingine kwa misingi ya sifa na hulka zilizopo. Hapa, sifa ya dhana mpya ilitokana na sifa za dhana asilia. Uhusiano huu pia ni wa kihistoria. Tazama mifano ifuatayo:

(5.3)

<i>Leksia zinazofanana</i>	<i>Maana awali</i>	<i>Mageuko</i>	<i>Tabia</i>
Beberu	Mbuzi wa kiume/ndhenge	Mkoloni	Usumbu
Kupe	Mdudu afyonzaye damu	Mtu mtegemezi	Utegemezi
Umeme	Miali ya mwanga mkali	Nguvu za stima au betri	Utoaji wa Mwangaza uandamwao na radi

Maana za leksia katika (5.3) zinahusiana kihulka na za leksia asilia. Kwa hivyo hatuna budi kueleleza sifa mkoloni ikiwa tunanua kupata kiini cha mabadiliko ya leksia beberu. Kwa mfano, waliwasumbua Wenyeji kwa kuwa nyanganya ardhi yao yenye rutuba, kuwatoza kodi, kutowaheshimu na kuwasumbua tu. Tabia yao ‘ilinuka’ kama anukavyo mbuzi wa kiume.

(iv) Uhusiano wa Ki-mahali

Uhusiano huu unahusisha dhana ya mahali. Mifano kutoka kwa data ni:

(5.4)

<i>Leksia</i>	<i>Maana awali</i>	<i>Maana Mpya</i>
Ulingo	Jukwaa la kulindia shamba	Jukwaa la michezo
Uga	Uwanja mbele ya nyumba, Mahali wazi mjini	Uwanja maalum wa kuchezea Sehemu ya kuchezea dansi.

Hapa, sifa ya mahali fulani inahusishwa na nyingine inayoshahabiana na kuzalisha leksia mpya yenye maana tofauti.

(iv) Uhusiano wa Ki-mwendo

Huu ni uhusiano unaohusisha mwendo na upande ambapo kitu kinaeleke. Mwendo wenye we unaweza kuwa halisi au wa kidhahania. Kwa mfano maana ya awali ya leksia ya kale ‘tamba’ ilikuwa *kutembea au kusafiri*. Maana ya kisasa ni *usimulizi wa hadithi*. Mtambi au mtambaji ni mtu anayesimulia hadithi. Usafiri hupatikana katika hadithi kwa namna zifuatazo:

- (i) Masimulizi mengi ya Waswahili yalisheheni motifu za safari kama ile ya jagina Liyongo katika *Utendi wa Fumo Liyongo*, ubeti 8 hadi wa 33. Liyongo aliandikiwa waraka na mfalme asafiri Pate ili Wagalla

wamwone. Alitumia siku mbili pekee kusafiri kutoka Shaka hadi mjini badala ya siku nne ilivyokuwa desturi.

- (ii) Mtambaji huwasafirisha hadhira yake ulimwengu wa kidhahania au wa kidoto.
- (iii) Watambaji wengi pia huwa na tabia ya kutembea hapa na pale jukwaani wanapotamba hadithi kama mbinu ya kufaninikisha uwasilishaji wao.

Leo hii –tamba humaanisha ‘jiringa au jisifu, *enda huku na huko kwa kujigamba*’ na pili, *simulia* hadithi (TUKI 2013).

(vi) Uhusiano wa Kiwango au wa Ki-hesabu

Huu ni uhusiano unaotokana na kiwango cha kitu au hesabu yake. Umbo **mwe** lilikuwa katika hesabu ya Kiswahili cha kale kama sinonimu ya moja au mosi (Polome 1967:130). Pia hupatikana katika leksia ‘pamwe’ [pa + mwe] ambalo huwa na maana ya ‘pamoja’. Leksia pamwe hutumika kuelezea umoja wa kufanyika kwa jambo. Mabadiliko ya –mwe yanaashiria ‘ushirikiano’ na ‘umoja wa nia; kati ya wahusika na sio idadi ya wahusika. Leksia *umoja* ilitokana na idadi moja (mosi, -mwe). Huwa na maana msingi ‘hali ya kuwa moja tu.’ Hata hivyo si idadi tu hurejelewa katika dhana ya umoja bali pia husheheni umoja wa kihisia na kisaikolojia, utangamano, ushirikiano na uzalendo. ~ *wa Afrika Mashariki* au ~ *wa Afrika*. Katika mfano huu, dhana ya awali ni hesabu ya moja tu lakini dhana mpya ina maana ya ziada ya kisiasa yaani ‘kuwa na muungano’. Nayo leksia *wanga* ilipewa maana tatu katika Krapf (1882):

- (i) Kukata k.m. kuwanga mti (kukata mti).
- (ii) Kugonga kama vile wangwa na kichwa.
- (iii) Kuhesabu

Maana ya kwanza ya Krapf (ibid) inaashiria kukatakata mti katika vipande kadhaa. Kuhusu fasiri (ii) Krapf anaeleza kuwa *mtu hugongesha vidole anapohesabu*. Basi inaonekana maana (iii) inahusiana na maana (i) kuititia uhamisho wa kisitiari unaohusiana na kiwango na hesabu. Fauka ya hayo nambari zimehawilishwa kuyapa majina aina mbalimbali za mashairi kwa msingi ya idadi ya mishororo katika kila ubeti; *utatu* (tathlitha), *unne* (tarbia), *utano* (takhmisa), *usita* (tasdisa) na kadhalika. Basi nambari husika zimepata maana ya ziada kwa kuhusisha idadi ya mishororo na hisabati. Katika sehemu inayofuata tumejadili athari au matokeo ya mabadiliko ya maana za leksia katika lugha ya Kiswahili.

Athari za Sitiari Katika Mfumo wa Maana katika Kiswahili

Mabadiliko ya maana za leksia kuititia mbinu ya sitiari yana athari anuwai katika mfumo wa maana katika lugha ya Kiswahili. Makala haya yanajadili athari nne kuu. Kwanza ni kuzuka kwa upolisemia ambao hatimaye husababisha utata wa kileksia. Utata hutokeea ikiwa maana mpya itaendelea kutumika sambamba na

maana ya awali. Aliye na umilisi wa lugha huenda akatatizika kutambua kwa wepesi maana inayolengwa iwapo muktadha mwafaka hautajengwa. Tazama mifano ifuatayo:

- (i) Nimeona kiboko.
- (ii) Nimepata jiko.
- (iii) Tulitamba

Katika mifano hii, hali mbili huenda zikazuka. Kwanza, ni kuona vigumu kuteua maana iliyokusudiwa na pili, kuteua maana tofauti na inayolengwa na msemaji. Uteuzi wa maana hutegemea tajriba na maaarifa, muktadha na matarajio ya mpokezi. Leksia *kiboko* ikitajwa, huenda afisa wa pori akajinashibisha na maana ya mnyama *mnene wa majini*. Huenda mwalimu na askari watajinashibisha na maana *mjeledi* au mnyama huku mtaalamu wa kuthibiti uzito akiteua *mtu mkubwa*. Katika (ii) mpokezi atatatizika kuteua *kifaa cha kupika* au *mke* na katika (iii) kuna utata wa kuteua maana *usimulizi wa hadithi* au *tembea kwa majisifu*. Polisemia ni chanzo mojawapo cha makosa katika lugha.

Athari ya pili ni kuongezeka kwa lugha ya kitaswira katika lugha. Kama tulivyodokeza mwanzoni, sehemu kubwa ya lugha inayotumika na binadamu ni sitiari. Sitiari huwa mojawapo ya mbinu ya kuzalisha maneno katika lugha kwa kuhamisha dhana kwa nyingine kianalojia. Mbinu hii hutegemea picha za kimawazo. Kinachohamishwa huwa tabia, taswira ya umbo au kazi ya kitu kwa kuihusisha na tabia au umbo au kazi ya kitu kingine. Kipacha (2005:102) anasema kuwa sitiari ina muundo ufuatao: mada (kizungumzwa), taswira (kifananishi) na ufanano (kiungo). Zingatia jedwali lifuatato:

Jedwali 2: Mada, taswira na ufanano

Mada (Kizungumziwa)	Taswira (Kifanishi)	Ufanano (Ufanano)
Gari la kivita	Kifaruu	Nguvu, umbo
Msichana	Kipusa	Thamani, urembo
Chombo cha usafiri	Ndege	Umbo, kuele angani
Stima	Umeme	Mwangaza
Kiingilio	Mdomo	Uwazi, upenyo
Uongozi	Simba	Ujasiri
Mke	Jiko	Upishi
Mitambo wa kupiga hewa	Uyoyozi	Hewa baridi, utulivu
Riziki	Unga	Hulisha mtu
Bidii	Jasho	Huzalisha riziki

Katika mifano hii, sitiari au lughā ya kitaswira ilihuksika kuleta mabadiliko yanayotokana na ufanano wa aina fulani. Kuhusu *kifaru* taswira ya maono kuhusu mnyama huyu inahusu kiumbe mnene aliye na upembe katika uso wake inayofanana na umbo la gari la kivita la wanajeshi wa ardhini ambalo huwa na mzinga mkubwa katika uso wake. Katika sitiari hii, *uso wa kifaru* unalinganishwa moja kwa moja na *uso wa gari* la kivita ambapo mwelekeo wa dhana unaakisiwa. Basi taswira ya *kipusa* cha kifaru inahamishiwa katika dhana mpya ya *msichana mrembo*. Wanasemantiki tambuzi hudokeza kuwa maarifa ya kiutambuzi huwa katika kategoria zenye mipaka ambayo ikipanuka, mabadiliko ya kisemantiki hutokeea. Kuhusu leksia *ndege* (nyuni, kikale), mambo manne muhimu yaliyosaidia kujenga taswira iliyozalisha leksia *ndege* (chombo cha angani):

- (i) Huwa na umbo lililochongoka mbele kama ule wa mshale.
- (ii) Huwa na mabawa mawili.
- (iii) Huwa na uwezo wa kupaa na kusafiria angani.
- (iv) Huwa na miguu miwili.

Pia katika baadhi ya mazingira ya Waswahili miale ya mwangaza ilioandamana na ngurumo katika misimu ya mvua iliitwa *umeme* (Nabhany 2012). Majilio ya betri na stima yalizimbua maarifa katika utambuzi yaliyojenga taswira iliyooana na umeme. Ujuzi huu ulihamishwa hadi kwa dhana mpya huku maana asilia ikididimia. Aidha, taswira ya maono ya *mdomo* kama sehemu ya kuingizia chakula ilisababisha jazanda ya mahali penginopo pa kuingilia kama vile cha chupa kuitwa *mdomo wa chupa*. Wanaismu tambuzi hueleza kuwa maana imejikita katika maumbile ya binadamu yakiwa msingi wa kufasiri dhana katika ulimwengu wake. Pindi mabadiliko ya leksia yanapoongezeka ndivyo kiwango cha lughā ya kitamathali inavyozidi kuongezeka.

Mwisho, mabadiliko ya kisitiari husababisha kutoweka au kuffia kwa baadhi ya leksia. Mara nyingine leksia mojawapo hutoweka au kupunguza matumizi yake, hasa maana mpya inapotumika kama kuwakilisha dhana-mwiko. Kwa mfano maana ya awali ya ngono, ilikuwa ‘usingizi’kutokana na kitenzi ‘gona’ - kulala usingizi mnono (Krapf 1882). Kitenzi hiki pia hupatikana katika lughā za Kibantu k.v. Kikamba, Kimeru, Kikuyu na Kiembu kwa maana hii hii. Katika Steere (1870) ngono ni zamu ya mke kulala na mumewe. Krapf (*ibid*) anaeleza kuwa zamu ya suria inapofika ya kwenda chumbani mwa bwanake kumpa ushirika wa kitanda, ilisemekana kimafumbo kuwa anampa ngono (usingizi). Katika Kiswahili cha karne ya 21, ngono ni tendo la mwanamke na mwanamume kujamiiiana. Maana asilia imetoweka.

Pia, utashi wa mwanadamu wa kupenda vitu vipyta tu. Matumizi ya muda mrefu wa leksia humsinya. Kwa mfano nafasi ya leksia ya kale mshekuu kuchukuliwa na mkopo alfajiri. Msomaji wa matini zenye Kiswahili cha kale

anakumbana na idadi kubwa ya leksia ambazo ni geni kwake na ambazo zimewekwa pemberi na wazungumzji wengi wa Kiswahili Sanifu.

Hitimisho

Makala haya yamejadili nafasi ya sitiari katika mabadiliko ya kisemantiki ya leksia za Kiswahili kwa kulinganisha mifano mahususi ya Kiswahili cha kabla ya Karne ya Ishirini na Kiswahili cha Karne ya Ishirini na Moja. Imebainika wazi kuwa mbinu ya sitiari imechangia pakubwa katika kuunda maneno mapya na kubadilisha muundo wa maana katika Kiswahili. Makala haya pia yameshughulikia mahusiano kati ya maana za leksia za awali na za kisasa. Mahusiano yaliyobainika yamekitwa katika umbo, tabia, matumizi, mahali, mwendo na idadi. Aidha, makala haya yamejadili athari za sitiari katika muundo wa lugha ya Kiswahili. Imekuwa wazi kuwa sitiari husababisha utata kupita kuzua maneno yenye sifa ya kipolisemia, kuongezeka kwa lugha ya kitaswira na kusababisha baadhi ya leksia kutoweka au kufifia.

Imebainika kuwa mwanadamu ana uwezo mkubwa wa kuhamisha maana kutoka wanda moja la maarifa hadi jingine kuitopia lugha ya kitaswira na kuthibitisha kauli kwamba sehemu kubwa ya lugha ni sitiari. Pindi jamii nzima inavyobadilika kutohana na maendeleo ya sayansi, teknolojia, uchumi, kijamii na kisiasa, ndivyo pia nafasi ya sitiari inavyozidi kuimarika katika juhudzi za kuzalisha leksia mpya.

Marejeleo

- Abdulaziz M. H. (1979). *Muyaka 19th Century Swahili Popular Poetry*. Nairobi: Kenya Literature Bureau.
- Burt, F. (1910). *Swahili Grammar and Vocabulary*. London. Society For Promoting Christian Knowledge Northumberland Avenue, W.C.
- Chiraghdin S. (1987). *Malenga wa Karne Moja*. Nairobi: Longman Kenya limited.
- E.A.E.P. (2011). *Comprehensive Swahili – English Dictionary*. Nairobi: E.A.E.P. limited.
- Hichens, W. (1939, 1972). *Al-Inkishafi: The Soul Awakening*. Nairobi: Oxford University Press.
- Kipacha, A. (2005). Utangulizi wa Lugha na Isimu. OSW 101. Dar es Salaam: Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.
<https://www.researchgate.net/publication/305807373> (pdf document).
- Knappert, J. (1979). *Four Centuries of Swahili Verse*. London: Hinemann.
- Krapf, J. L. (1850, 1882). *Dictionary of Suaheli Language*. London: Trubner and Co. Ludgate Hill.
- Krumm, B. (1940). *Words of Oriental Origin in Swahili Language*. London: The Sheldon Press.

- Lakoff, G. (1987). *Women, Fire, and Dangerous Things*. University of Chicago Press. Chicago.
- Lemmens, M. (2017). A Cognitive , Usage-based View on Lexical Pragmatics in I. Depraeter & R. Salkie (eds) *Semantics and Pragmatics: Drawing line*. Springer, Cham 101-114.
- Longhorn Publishers (2011). *Kamusi ya Karne ya 21*. Nairobi. Longhorn Publishers.
- Mulokozi, M. M. (Mha.). 1999. *Tenzi Tatu za Kale*. Dar es Salaam: TUKI.
- Mutiso, K. (2005). *Utenzi wa Hamziya*. Dar es Salaam: TUKI
- Nabhany, S. A. (2012). *Kandi ya Kiswahili*. Dar es Salaam: Aera Kiswahili Researched Products.
- National Museums of Kenya (2005). Interactive Project: Swahili Attire Exhibition. Nairobi: NMK.
- Polome, E. (1967). *Swahili Language Handbook*. Washington: Centre for Applied Linguistics.
- Steere, E. (1870). *A Handbook of the Swahili Language as Spoken at Zanzibar. Revised Edition by Madan (1919)*. London: Society for Promotion of Christian Knowledge.
- TUKI. (2004, 2013). *Kamusi ya Kiswahili Sanifu*. Nairobi: Oxford University Press.
- Vyvyan et al (2006). ‘The cognitive Linguistics Enterprise: An Overview’ in *The Cognitive Linguistic Leader*. London: Equinox publishing Company.